Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# MUHTASARI WA MATOKEO YA TAFITI ZILIZOFANYWA NA OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO KWA MWAKA 2008/09

## AWAMU YA PILI

**Ofisi ya Rais,**
**Tume ya Mipango**

**JANUARI, 2010**

## 6.0 MABADILIKO YA IDADI YA WATU KATIKA MAENDELEO YA KIUCHUMI

### *6.1 Chimbuko*

Tafiti nyingi zilizofanyika zimeonyesha kuwa kuna mahusiano ya karibu sana kati ya ongezeko la ukuaji wa idadi ya watu na ukuaji wa kiuchumi. Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2006 inafafanua kuwa katika kipindi cha muda mfupi madhara ya ukuaji wa idadi ya watu yanaonekana kuwa madogo lakini katika kipindi muda wa kati na mrefu madhara yatakuwa makubwa zaidi na yanaathiri nyanja mbalimbali zinazochangia ukuaji wa uchumi. Hii ni kwa sababu vigeu (variables) vya idadi ya watu vinaathiri maendeleo ya hali ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla. Vigeu hivyo muhimu vinavyosababisha mabadiliko ya idadi ya watu ni uzazi, vifo/magonjwa na uhamaji. Ongezeko la kasi la idadi ya watu katika nchi yenye uchumi unaokua kwa kasi ndogo unaongeza matumizi zaidi katika kutoa huduma (mfano za elimu na afya) na hivyo kufanya serikali kupunguza matumizi katika shughuli nyingine za kuleta maendeleo endelevu mfano katika uwekezaji na kuongeza mitaji. Kwa kutambua umuhimu wa uhusiano huo, Tume ya Mipango kwa kumtumia mtaalamu mwelekezi “Data Works Associates Ltd” ilifanya utafiti wenye lengo la kuchambua na kushauri ipasavyo kuhusu mahusiano yaliyopo kati ya ukuaji kwa idadi ya watu na kukua kwa uchumi wa taifa.

### *6.2 Lengo la utafiti*

Lengo kuu la utafiti huu ni kuhusisha na kuchambua vigeu muhimu vya idadi ya watu (katika muda mfupi, kati na mrefu) na maendeleo ya uchumi ili kuwezesha Tanzania kuwa na uchumi imara na wa ushindani ifikapo mwaka 2025.

### *6.3 Matokeo ya Utafiti*

Matokeo ya utafiti yamebainisha yafuatayo;

i) Kiwango cha vifo vya watoto nchini Tanzania vinapungua wakati kiwango cha uzazi bado kiko juu hali inayosababisha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu. Hali hii isipodhibitiwa itafanya idadi ya watu kuongezeka hadi kufikia watu milioni 63 ifikapo mwaka 2025;

ii) Umri wa kuishi wa Mtanzania umeathiriwa kwa kiasi kikubwa na Malaria na VVU/UKIMWI. Athari za VVU/UKIMWI pia zinajionesha katika kupungua na kudhoofika kwa nguvu kazi na hivyo kuongezeka kwa kiwango cha utegemezi;

iii) Suala la wahamiaji wa kimataifa halijapewa uzito wa kutosha kutokana na kutokuwepo kwa taarifa zinazowahusu. Taarifa zilizoko ni zile za wakimbizi tu;

iv) Tanzania imekuwa ikiandaa sera za kisekta, mikakati na programu zinazolenga kuboresha usimamizi wa idadi ya watu na ukuaji wa uchumi. Hata hivyo, sera, mikakati na programu hizo hazijatekelezwa ipasavyo kutokana na uratibu duni na mfumo usiojitosheleza kisheria.

### *6.4 Mapendekezo ya Mtaalamu Mwelekezii*

Ili kuiwezesha Tanzania kufikia uwiano sahihi baina ya idadi ya watu na maendeleo ya kiuchumi mtaalam mwelekezi alipendekeza yafuatayo:

i) Kuchukua hatua za makusudi za kupunguza kiwango cha uzazi na vifo vya watoto;

ii) Kuwepo na mipango, sheria na kanuni za udhibit katika muda mfupi, wa kati na muda mrefu;

iii) Kuelekeza rasilimali za kutosha katika kuboresha afya ya Uzazi;

iv) Kuwepo na mchakato endelevu wa kuboresha elimu kuhusu lishe hasa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano;

v) Kuweka mikakati ya kubadili tabia na mienendo ya watu ikiwa ni pamoja na uangalizi wa waliokwisha athirika;

vi) Ongezeko la idadi watu litumike kama fursa ya kuchochea maendeleo kwa;

- Kwa kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo
- Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;
- Kuwajengea vijana uwezo ili kuimarisha nguvukazi yenye tija
- Kuboresha huduma za hifadhi za jamii na afya kwa wazee;
- Mfumo wa ukusanyaji wa Takwimu muhimu uimarishwe kwa kuanzisha rejista za idadi ya watu katika ngazi ya kijiji, kata na wilaya.

### *6.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango*

Kitaalam inapendekezwa kuwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kinapaswa kuwa mara tatu zaidi ya kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu. Kutokana na kiwango cha sasa cha ukuaji wa idadi ya watu cha asilimia 2.9, kiwango cha ukuaji wa uchumi kinatakiwa kuwa zaidi ya asilimia 9. Hivyo, tunapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe;

i) Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi;

ii) Elimu kwa wote iendelezwe kufikia angalau hadi kidato cha nne ili kuwezesha vijana kuelewa mbinu mbalimbali za kuyamudu maisha na kupunguza ndoa na mimba za umri mdogo;

iii) Serikali iendelee kuboresha miundombinu ya kiuchumi ili kupanua fursa za kuongeza wigo wa ushiriki wa jamii katika uchumi na hivyo kuongeza ajira; na

iv) Kubuni mbinu endelevu za kuwajengea vijana uwezo kwa lengo la kutumia nguvu kazi iliyopo kama rasilimali.

## 7.0 TIJA YA UZALISHAJI KATIKA SEKTA ZA UZALISHAJI NCHINI TANZANIA NA USHINDANI WA BIDHAA ZAKE KWENYE MASOKO.

### *7.1 Chimbuko*

Dira ya Taifa ya maendeleo; pamoja na mambo mengine imelenga kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania, kujenga uchumi imara wenye kuhimili ushindani na hivyo kwa Tanzania kushiriki ipasavyo katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Sekta za uzalishaji zikiwemo kilimo, viwanda, madini, uvuvi, misitu nyuki na wanyamapori zina umuhimu wa kipekee katika uchumi wa Tanzania. Ni chanzo kikuu cha ajira na kipato kwa zaidi ya asiimia 90 ya Watanzania wote na zinachangia zaidi ya asilimia 50 ya Pato la Taifa (GDP).

Sekta za uzalishaji nchini zina fursa tele ambazo kama zingetuimika ipasavyo, sekta hizo zingeweza kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye maendeleo ya uchumi na jamii kuliko inavyochangia sasa. Hili litawezekana kama itakuwepo mikakati madhubuti itakayolenga kuinua tija ili hatimae kuongeza uzalishaji na kuzalisha bidhaa bora zenye ushindani kwenye soko.

Kwa maana hiyo, mafanikio ya malengo ya Dira ya Taifa yanategeme sana ufanisi utakaokuweza kupatikana katika sekta za uzalishaji. Kwa kuzingatia hoja hizo, Tume ya Mipango ilimtuma mshauri mwelekezi (Kampuni ya Innovex Development Consultants Ltd) kufanya utafiti juu ya jambo hili.

### *7.2 Madhumuni ya Utafiti*

Madhumuni ya utafiti huu ni kubainisha endapo na kwa kiwango gani kiwango cha tija ya uzalishaji pamoja na ushindani wa bidhaa za sekta hizo kwenye soko vilivyo vya chini hapa Tanzania ikilinganishwa na

nchi nyingine duniani; na vilevile kubaini sababu za unyonge huo kwa uchumi wa Tanzania na hatimae kuweza kupendekeza hatua na mikakati itakayowezesha kupatikana ufumbuzi wa tatizo hilo.

### *7.3 Matokeo ya Utafiti*

**i) Kilimo**

- Kiwango cha uzalishaji wa mazao makuu ya chakula na biashara kimeshuka,
- Sehemu kubwa ya kil imo  Tanzania inafanywa na wakulima wadogo wakiwa na vishamba vidogo visivyokuwa na tija,
- Sehemu kubwa ya kilimo nchini inafanyika kwa kutumia teknolojia duni ikiwa ni pamoja na kutegemea mvua na kutumia zana duni kuanzia kulima, kutunza, kuvuna na kuhifadhi mazao,

- Kilimo cha umwagiliaji kinachukua sehemu ndogo sana ya kilimo cha Tanzania,
- Utafiti wa kilimo unaofanyika nchini ni kidogo sana. Aidha matumizi ya sayansi na teknolojia kwenye kilimo nchini nayo ni kidogo sana..

**ii) Misitu**

Ushirikishwaji wa serikali za mitaa kwenye usimamizi wa serikali za mitaa ni hafifu.

**iii) Uvuvi**

Kuna usimamizi hafifu kwenye rasilimali za uvuvi, hasa  katika ukanda wa eneo huru la bahari.

### *7.4 Uzalishaji Viwandani*

**i) Sekta ya viwanda inakabiliwa na changamoto zifuatazo**

- Uhaba wa wataalaam wenye wenye ujuzi na ubunifu,
- Viwanda vingi has vidogo na vya kati vinatumia teknolojia duni na iliyopitwa na wakati,

- Bidhaa za viwanda vingi nchini zinakabiliwa na ushindani mkali kwenye soko la ndani unaotokana na wingi wa bidhaa za kutoka nje zinazouzwa kwa bei ndogo japo bidhaa hizo zikiwa hazina ubora unaostahili,
- Huduma hafifu za miundombinu (mfano za ucheleweshaji bandarini, ukosefu wa umeme wa uhakika n.k) zinachangia katika kupungua kwa uzalishaji pamoja na gharama za uzalishaji kuwa juu,

***ii) Madini***

- Wageni wamehodhi sekta ya uchimbaji mkubwa wa madini huku wenyeji wengi wanaoshiriki kwenye sekta hii wakibakia kwenye uchimbaji mdogo,
- Mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa bado ni mdogo,
- Mwingiliano (linkage) kati ya sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi ni mdogo.

### *7.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango;*

- Mengi ya mapendekezo yaliyotolewa tayari yamo katika mikakati na program zinazoendelea kutekelezwa na serikali.
- Aidha ripoti haina mapendekezo yaliyo makini nay a kutosheleza kutatua matatizo sugu ya sekta za uzalishaji. Kwa mfano hakuna pendekezo la kisera au hata kiprogram kwa ajili ya kushugulikia matatizo sugu ya nishati na bandari.
- Hakuna mapendekezo maalum kuhusu namna ya kuinua tija kwenye sekta mbalimbali.
- Kufuatia mapungufu yaliyojitokeza katika Ripoti hii, kuna haja ya kuandaa zoezi jingine kwa ajili ya kuziba mapengo yaliyopo ili kupata mapendekezo imara ya jinsi ya kufanikisha Mapinduzi ya kilimo nchini.

## 8.0 UTAFITI KUHUSU HATUA ZINAZOHITAJIKA KULETA MAPINDUZI YA KILIMO NCHINI

### *8.1 Chimbuko*

Kilimo kinachukua nafasi ya pekee kwa ustawi na maendeleo ya Watanzania walio wengi. Asilimia 80 ya Watanzania wanatyegemea kilimo kwa maisha yao. Kilimo ni mchangiaji mkubwa kwenye pato la Taifa ambapo mwaka 2007 kilkimo kilichangia asilimia 25.8 ya pato la Taifa. Pia ni mchangiali mkubwa wa mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya bidhaa za kilimo nchi za nje. Aidha Kilimo ndiyo chanzo kikubwa cha ajira pamoja pamoja na chakula kinacholiwa nchini

Tanzania inazo fursa nyingi za kuweza kuendeleza kilimo (zikiwemo rasilimali asilia na sisizo asilia ardhi bora na kubwa, hali y hewa, maji, masoko n.k.). Kwa sasa Tanzania inatumia sehemu ndogo ya fursa hizi. Ni sahihi pia kusema kwamba mchango wa sekta ya kilimo kwa maendeleo ya Tanzania ni mdogo sana kwa vile umetokana na matumizi madogo mno ya fursa zilizopo. Hata hivyo kwa sekta ya kilimo kuongeza mchango wake kwa kiwango cha kutosha itateegemea sana maendeleo katika kuongeza ufanisi kwenye sekta hiyo ambavyo kwa sasa ni jambo la wazi kwamba kiwango cha ufanisi kiko chini mno.

Mifano kutoka mahali pengi inaonyesha kwamba ili kuongeza ufanisi na kufanikisha kilimo, ni lazima kufanya mapinduzi kwenye sekta hiyo. Katika jitihada za kuona endapo na ni vipi Tanzania inaweza kufanikisha mapinduzi ya kilimo, Tume ya Mipango ilimtafuta na kumpata Mshauri Mwelekezi **( TISCO Consultants Ltd** na kumpa kazi ya kulifanyia utafiti eneo hilo.

### *8.2 Lengo na Madhumuni ya Utafiti Uliofanyika*

Lengo na madhumuni ya utafiti huu ni kubaini uwezekano na jinsi gani/mbinu zinazoweza kutumiwa ili kuleta mapinduzi ya kilimo nchini Tanzania kama

mkakati wa kukuza mchango wa sekta hiyo kwenye uchumi wan chi na maendeleo kwa jumla.

### *8.3 Matokeo ya Utafiti*

Utafiti uliofanyika umebainisha kwamba;

i) Tija katika sekta ya kilimo hususan katika uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini Tanzania iko chini sana hata ukilinganisha na nchi nyingi duniani zikiwemo nchi za jirani barani Afrika zikiwemo Malawi, Kenya na Afrika ya Kusini,

ii) Sehemu kubwa ya kilimo ni kilimo cha wakulima wadogo ambao wanatumia teknolojia duni, (njia duni, zana duni na matumizi kidogo mno ya mbolea); na hivyo mavuno yao kuwa tofauti mno na yale yanayopatikana kwenye miradi ya utafiti (inayotumia teknolojia bora,

iii) Wakati maji ni nyenzo muhimu mno kwa kilimo, sehemu kubwa ya kilimo cha Tanzania ni cha kutegemea mvua ambayo ni chanzo cha maji kisichokua na uhakika,

iv) Wakulima wengi nchini hasa wale wadogo wanashindwa kupata huduma za uwezeshhaji kiuchumi na hivyo kushindwa kuwekeza na kuboresha shughuli zao ipasavyo kutokana na uwezo mdogo na taratibu ngumu zilizowekwa na taasisi zilizopo zinazotoa huduma hizo,

v) Ufinyu wa miundombinu ya usafiri, mawasiliano, maghala ya kuhifadhia mazao ni kizingiti kikubwa katika jitihada za kuboresha kilimo nchini,

vi) Ka muda mrefu sasa kilimo nchini Tanzania imekua ni kazi yenye faida kiduchu na gharama kubwaza uzalishaji kwa wakulima wengi kutokana na sera hasi za kilimo,

### 8.4 Mapendekezo ya Mtaalam Mwelekezi

Katika Ripoti hii Mtaalam Mwelekezi amependekeza mambo yafuatayo ili kufanikisha mapinduzi ya kilimo Tanzania;

i) Kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wazalishaji na kuvijengea uwezo vyama vya ushirika ili kukuza shughuli za kilimo,

ii) Kwa kushirikiana na sekta binafsi kuimarisha taasisi za utafiti na kuhakikisha kuwa taarifa za matokeo ya tafiti zinawafikiwa wakulima na kwa wakati
iii) Kuboresha huduma za ughani kwa kuajiri na kutoa mafunzo ya maramara kwa maafisa ughani,
iv) Kuboresha miundombinu ya usafiri(barabara, reli na maji) hasa kwa maeneo ya vijijini na kuhimiza ujenzi wa maghala ya kuhimiza mazao,
v) Kuharakisha uanzishwaji wa Bank ya Kilimo ili wakulima waweze kupata mikopo kwa ajili ya shughuli za kilimo,
vi) Kuboresha usambazaji wa pembejeo kwa wakulima kwa kuimarisha mfumo wa vocha,
vii) Kuimarisha huduma ya ukaguzi wa mazao na kuanzisha maabara ili kuhakikisha kuwa mazao yanakidhi viwango na ubora unaokubalikakatika masoko ya nje,
viii) Kuhimiza ushirikiano baina ya wazalishaji wadogo na wasindikaji ili kuwa na uhakika wa soko,
ix) Kuwepo na mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuainisha maeneo ya umwagiliaji kwa wakulima binafsi,
x) Kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya maji, na,
xi) Kuanzishwe Bima ya Kilimo ambapo wakulima watakua na uhakika wa mapato hata inapotokea mabadiliko ya hali ya hewana kuathiri mazao.

## 8.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango

Baada ya kupitia na kuchambua Ripoti hii Tume ya Mipango ina maoni na mapendekezo yafuatayo;

i) Maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Mtaalam Mwelekezi yote ni muhimu kwa ufanikishaji ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini,
ii) Mengi ya maoni na mapendekezo yaliyotolewa kwenye utafiti huu ni kama yanakazia maoni na mikakati ambayo tayari yapo na yanatekelezwa labda tu kwa kiwango ambacho bado hakitoshaelezi,
iii) Hata hivyo, baadhi ya masuala yaliyoibuliwa katika utafiti huu hayakuweza kuchambuliwa kwa undani,

iv) Pia kuna masuala machache (ambayo yanafahamika kuwa ni masuala nyeti kwa kilimo) ambayo Ripoti hii haikuyatazama na hivyo kushindwa kuyatolea mapendekezo yoyote,

v) Kwa sababu ya uchambuzi uliofanyika haukuweza kugusa baadhi ya masuala muhimu kuhusiana na apinduzi ya kilimo,

vi) Kwa sababu ya mapungufu yaliyojitokeza kama yalivyotajwa katika 2), 3) na 4), maoni na mapedekezo yaliyotolewa katika Ripoti hii hata kama yatatekelezwa bado haitakuwa njia tosha kuleta mapinduzi ya kilimo,

vii) Wakati maoni (findings) yalipaswa kuwa ndiyo msingi muhimu wa Mapendekezo ya nini kinatakiwe kifanyike kufanikisha mapinduzi ya kilimo, katika utafiti huu mapendekezo hayaonekeni kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maoni. Kwa mfano kuwapo kiwango kidogo cha tija, matumizi makubwa ya zana duni na matumizi madogo mno ya mbolea ni kati ya masuala yaliyoonekana lakini katika mapendekezo hakuna yaliyotolewa kwamba ni nini kifanyike kupata ufumbuzi wa unyonge huo ulotajwa,

viii) Mapendekezo yetu ni kwamba serikali iyakubali mapendekezo yaliyokwisha tolewa na kuagiza vyombo husika kuona namna ya kuyatekeleza,

ix) Pia, kwa vile kuna masuala mengi muhimu ambayo hayajaibuliwa na kufanyiwa uchambuzi wa kina, Tume tunaonelea ni muhimu kuehdeleza utafiti wa suala zima la mapinduzi ya kilimo ili kuweza kupata mapendekezo mazuri zaidi na ya kutosha kwa azma hii (kwa kuwatumia watafiti wengine mahili zaidi).

## 9.0 TANZANIA ITAENDANA NA KUFAIDIKA VIPI NA UTANDAWAZI

### *9.1 Chimbuko*:

Utandawazi ni matokeo ya mchanganyiko wa athari za biashara zilizolegezwa masharti, mchanganyiko wa masoko, usimamizi wa kimataifa wa fedha na uwekezaji, mabadiliko ya teknolojia, kuongezeka kwa usambazaji wa bidhaa kuvuka mipaka ya nchi moja kwenda nchi nyingine na kutokea kwa muundo mpya wa kidunia wa mtazamo wa utawala. Utandawazi pia unaweza kurahisishwa au kuchochewa na sera za serikali. Katika eneo hili tafiti nyingi zimefanyika kitaifa na kimataifa ili kusaidia nchi kuweza kushiriki kikamilifu katika utandawazi. Hata hivyo inaonyesha kuwa kuna haja ya kufanya utafiti kwa Tanzania ili kuona ifanyeje ili iweze kujihusisha zaidi katika biashara ya kimataifa.

### *9.2 Malengo*

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchambua ushiririki wa Tanzania katika biashara ya kimataifa ili kubaini ni kwa jinsi gani Tanzania itaweza kushiriki katika mapatano ya biashara. Masuala ya msingi katika utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kuangalia;

- Ni mambo gani ambayo yanasababisha Tanzania kutoshiriki vyema katika biashara ya kikanda na kimataifa,
- Changamoto za ndani na nje ya nchi na
- Ni kwa namna gani Tanzania itaweza kushiriki katika biashara ya kimataifa kwa kuainisha vizuizi ambavyo vinaweza kusababisha Tanzania isifaidike katika biashara ya kimataifa. Vilevile kuainisha sehemu za kutiliwa mkazo katika muundo wa taasisi husika ili kusaidia ushiriki wa Tanzania katika biashara ya kimataifa.

## 9.3 Matokeo ya Utafiti

i) Mwenendo wa Biashara

- Kuongezeka kwa mauzo nje na kuongezeka kwa bidhaa zisizo za asili;
- Kuongezeka kwa nchi ambazo zinafanya biashara na Tanzania; Tanzania imeongeza mauzo yake nje na hasa katika jumuiya za EAC, SADC, EU pamoja na nchi nyingine zinazoibukia kiuchumi;
- Uongezekaji wa bidhaa ("intermediate and capital") kutoka nje kama moja ya matokeo ya kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta za madini, utalii na uzalishaji (manufacturing);

ii) Utandawazi na Manufaa yataokanayo na Biashara ya Kimataifa

- Ingawaje Tanzania inaweza kushirika katika masuala ya utandawazi, lakini maoni ya wadau ni kuwa bado nchi haijanufaika sana na utandawazi;
- Kushindwa kutumia fursa zitokanazo na ushirikiano wa kikanda na makubaliano ya biashara za kimataifa;
- Uchache wa aina ya bidhaa zinazouzwa nje;
- Ushiriki mdogo wa wauzaji wa bidha nje katika uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa wanazouza nje;
- Kiwango kidogo cha teknolojia ya uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje,
- Athari za mtikisiko wa kifedha duniani umesababisha kupungua kwa mauzo nje ya nchi;'
- Kuongeza kwa mapato kutokana na ushirikiano na makubaliano ya biashara kikanda na kimataifa;

iii) Vikwazo vya ushiriki wenye manufaa kwa Tanzania katika biashara ya kimataifa ni pamoja na:

- Kusuasua kwa utekelezaji wa mikakakti ya sera ya Taifa ya biashara;
- Uwezo mdogo wa uzalishaji,
- Ugumu katika taratibu za uingizaji na uuzaji wa bidhaa nje,

iv) Uwiano wa Sera ya biashara na sera nyingine za kitaifa

- Athari za sera zinazosaidia uhusiano na biashara katika biashara ya kimataifa
- Utekelezaji usioridhisha wa makubaliano ya mikataba ya kibiashara;
- Mapungufu ya sheria ya mamanuzi ya mwaka 2004; sheria hii imeshindwa kutoa upendeleo wa kipekee kwa wazalishaji wa ndani na hasa wadogowadogo; na
- Kushindwa kutumia vyema faida zinazopatikana kutokana na kupanuka kwa masoko.

## 9.4 Mapendekezo ya Mtaalam Mwelekezi

Mtaalamu mwelekezi aliyechaguliwa kufanya kazi hii ni Economic Research Bureau ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mapendekezo yake ni kama ifuatavyo;

i) Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika biashara ya kimataifa

Utafiti huu umebaini kwamba malengo ya sera ya taifa ya biashara ya 2003, yapo sawia na mahitaji ya ushiriki wa Tanzania katika biashara ya kimataifa. Sera hii inalenga kuongeza uwezo na kupanua muungiliano wa uzalishaji wa ndani na kujenga uwezo wa ushindani katika biashara ya nje kwa lengo la kukuza viwango vya ukuaji na maendeleo.

ii) Kuboresha na kuendeleza uwezo wa mazingira ya sera

Serikali ichukue hatua kuhakisha kwamba taifa linanufaika na fursa za masoko na kiuchumi zinazojitokeza katika mifumo ya biashara ya kimataifa na uwanachama katika taratibu za biashara za kikanda. Aidha utafiti wa kina ufanyike ili kubaini mikakati maalum ambayo inalenga mambo yafuatayo;

- Kuongeza mauzo ya nje ya bidhaa za asili na zisizo za asili

- Kuhamasisha uongezaji dhamani katika bidhaa za kuunza nje hasa katika maeneo ya kilimo, madini na utali kwa lengo la kuinua uwekezaji ktk viwanda.
- Kuhamasisha na kuelekeza uwekezaji wa kutoa n je na ndani kwenye mfumo wa kibiashara ambao utatumika kama kiungo au kiunganishi kati ya wazalishaji wa ndani na masoko ya kimataifa.
- Kuongeza na kuboresha sekta ya huduma za kisasa kwa kipaumbele kuhudumia mizingo ya nje na utali.

iii) Kuongeza washirika wapya wa kibiashara na kuendelea na wale wa zamani

iv) Kuchunguza na kutathimini masoko mapya

v) Kuongeza kiwango cha kuagiza bidhaa za kati na za mitaji

vi) Kuongeaza wigo wa uuzaji nje

vii) Kuondoa vikwazo vinavyokwamisha ushiriki wenye faida katika biashara ya kimataifa

viii) Kuongeza utekelezaji wa mikakati wa sera ya taifa ya biashara

ix) Kuongeza uwezo wa uzalishaji wa ndani

x) Kuimarisha uwezo na uwezeshaji wa taasisi katika ushiriki wa biashara ya kimataifa

xi) Kuimarisha utekelezaji wa makubaliano mkakati/mikakati

### 9.5 Mapendekezo *ya Tume ya Mipango*

i) Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 ifanyiwe mapitio ili kuzingatia masuala mabadiliko yaliyojitokeza;

ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iendelee kujenga uwezo katika ujuzi wa majidiliano miongoni mwa wataalam wa kitanzania;

iii) Serikali ijipange na kuwahamsisha wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu na kwa manufaa zaidi kwenye soko la pamoja la Afrika mashariki na fursa nyingine za kimataifa zinazojitokeza;

iv) Serikali ijenge uwezo wa uelewa miongoni mwa wadau kuhusu manufaa yanayotokana na utandawazi;

## 10.0 NAFASI NA ATHARI ZA RASILIMALI ZA NJE KATIKA UCHUMI

### *10.1 Chimbuko*

Tangu mwaka 1986 Tanzania imekuwa ikifanya marekebisho ya kiuchumi yenye nia ya kuendeleza ukuaji wa uchumi kwa kulegeza masharti ya soko. Haya marekebisho yameweza kwa kiasi kikubwa kuvutia rasilimali nyingi za nje kama Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja na Misaada ya Serikali ya Maendeleo. Hii misaada imekuwa ikitumika katika kuongezea akiba yetu ya ndani ambayo ni kidogo na kuleta pamoja nayo fedha, ustadi wa uongozi, teknolojia, utaalamu wa masuala ya masoko na kuunganisha katika masoko, ambayo haya yote yanahitajika sana katika kuendeleza uchumi.

Hata hivyo ingawa serikali inafanya marekebisho ya kiuchumi yanayounga mkono kuingia kwa rasilimali za nje katika uchumi, kuna wasiwasi juu ya manufaa (nafasi na athari) yake katika uchumi. Kwa hiyo imeonekana haja ya kupitia sera na mikakati ili kuweza kupata majibu ya maswali kuhusu mchango na athari za rasilimali za nje.

### 10.2 *Malengo*

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchambua nafasi ya rasilimali za nje katika uchumi kwa kuchunguza makubaliano ya kwenye mapitio ya vitabu kuwa rasilimali za nje zinasababisha utendaji mzuri wa uchumi.

### *10.3 Matokeo* ya Utafiti

i) Utafiti ulibaini kuwa Tanzania ni nchi iliyojaliwa wingi wa maliasili kama vile misitu, madani,wanyama, maji na raslimali watu. Rasilimali hizo kama zikitumiwa vizuri zinauwezo wa kuleta maendeleo ya haraka katika taifa na kupunguza mahitaji ya raslimali kutoka nje.

ii) Tanzania imeendelea kufanya maboresho katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo matokeo yake yamehamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za kiuchumi na upatikanaji na matumizi

bora ya mitaji kutoka nje.

iii) Tanzania imepiga hatua kubwa katika kubuni na kutekeleza sera zinazowawezesha wananchi kusimamia na kumiliki shughuli za kiuchumi na kijamii.

iv) Watanzania wanatambua juu ya marekebisho ya sera ya hivi karibuni, na wanaelewa, na wanataarifa za mchakato wa marekebisho ya sera na mchango wake. Hata hivyo baadhi hawajaelimishwa kwa kina undani wa miuundo na jinsi ya utekelezaji wa sera hizo.

v) Kwa kuzingatia uzoefu katika utekelezaji wa awamu ya kwanza na ya pili ya merekebisho jumla, serikali inatambua umuhimu wa mtazamo wa muda mrefu wa mipango ya maendeleo, na imefanya marejeo muhimu katika uchumi mdogo na sera za kisekta ambazo zinawezesha umilikaji, uwezeshaji na matumizi sahihi ya rasilimali za ndani.

vi) Tanzania imepata mafanikio makubwa katika uchumi jumla kuanzia katikati ya miaka ya 1980 hasa katika utekelezaji wa sera endelevu za mageuzi ya kiuchumi. Mageuzi hayo ya kisera yamekuwa ni kichocheo muhimu cha upatikanaji wa rasilimali kutoka nje na ndani ya nchi.

vii) Kutokuelekeza raslimali za kutosha kwa sekta zenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi kumefanya ukuaji wa uchumi kuwa mdogo pamoja na kuwepo kwa misaada mingi kutoka nje;

viii) Pamoja na kutokuwepo uwiano wa moja kwa moja kati ya misaada kutoka nje na ukuaji wa uchumi, ni dhahiri kuwa ukuaji wa uchumi utadorora kama misaada kutoka nje itasitishwa.

ix) Vikwazo vinavyozuia raslimali kutoka nje kutokuwa na mafanikio katika ukuaji wa uchumi wetu ni pamoja na mfumuko wa bei, nakisi katika bajeti, namna misada inavyotolewa, na ujumuishaji wa misaada katika mipango ya maendeleo.

x) Changamoto ya mitaji kutoka nje ni pamoja na;
Raslimali kutoka nje ili kusaidia kuziba pengo la raslimali zinazohitajika katika uchumi wa taifa kutokana na raslimali za ndani kuwa hazitoshi.

xi) Raslimali kutoka nje zimekuwa zikitumika kama mbadala wa raslimali za ndani badala ya kuziba pengo hivyo kuathiri ukusanyaji wa raslimali za ndani.

xii) Uwekezaji (FDI) kutoka nje kwa kiasi kikubwa umeelekezwa kwenye sekta ya madani ambayo muingiliano na sekta nyingine na mchango wake katika pato la taifa bado ni mdogo. Pamoja na mchango mkubwa unaotolewa na sekta ya kilimo na utalii katika pato la taifa bado uwekezaji wa mitaji kutoka nje katika sekta hizo ni mdogo. Hali hii ni uthibitisho tosha kuwa mitaji kutoka nje ina uhusiano mdogo na ukuaji wa uchumi.

xiii) Utafiti ulibaini kuwa fedha zinazokuja nchini kutoka kwa watanzania wanaofanya kazi nje ni kiasi kidogo sana kutokana na; kuwepo kwa idadi ndogo ya watanzania wanaofanya kazi nje,

xiv) kutokuwepo kwa tarifa za kutosha juu ya nafasi za kazi za kimataifa ambazo watanzania wenye sifa wangeliweza kuomba, na

xv) namba kubwa ya wafanyakazi wenye ujuzi mdogo.

### *10.4 Mapendekezo* ya Mtaalam Mwelekezi

Mtaalamu mwelekezi aliyechaguliwa kufanya kazi hii ni Economic Research Bureau ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mapendekezo yake ni kama ifuatavyo;

i) **Kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali**

Tafiti inashauri umuhimu wa kuendeleza matumizi bora ya maliasili ya ndani hususan madini kama njia ya kurekebisha uchumi na kupunguza umasikini.

ii) **Kuhimiza uendelezaji wa uchimbaji mkubwa wa madini unaomilikiwa na wazalendo**

Kuhimiza ushiriki wa wazawa katika uchimbaji mkubwa wa madini Katika eneo hili tafiti inashauri serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha na kuendeleza uchimbaji mkubwa wa madini utakaowahusisha sekta binafsi au sekta binafsi ikishirikiana na serikali (Public Private Partnership), kwani njia hii itaongeza ushiriki wa watanzania katika kumiliki raslimali zao. Vile vile sekta binafsi inaweza kushirikiana na wageni katika kuendeleza sekta hii ya madini(Joint venture).

Tafiti inashauri serikali kulijenga upya shirika la kusimamia maendeleo ya madini STAMICO nakulipa uwezo na nyenzo za kuwa huru kwa lengo la kuendeleza sekta ya madi hapa nchini.

iii) Kuendeleza utekelezaji wa mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa

iv) Tafiti inashauri kuwa Tanzania iongeze bidii katika utekelezaji wa mageuzi ya kuichumi, kijamii na kisiasa. Kuna haja ya kuendeleza mtengamano kati ya sera zinazotekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), MKUKUTA na Mkakati wa Misaada (Joint Assistance Strategy for Tanzania).

v) Kuimarisha utekelezaji wa sera za kupunguza umaskini

vi) Tafiti inashauri kuwepo kwa mazingira mazuri ya kutekeleza sera zenye lengo la kupunguza umaskini. Pale penye mazingira mazuri ya kisera, raslimali kutoka nje zinakuwa ni kichocheo cha kupunguza umaskini kwani zinatoa fursa ya raslimali hizo kutumika vizuri.

vii) Kuimarisha utekelezaji wa sera za Mpango Mkakati wa kuvutia vitegauchumi

viii) Kutokana na yaliyobainshwa na tafiti katika eneo hili, kuna haja ya kutekeleza sera za kuvutia mitaji kutoka nje kwa lengo la kuleta ufanisi katika ukusanyaji na utumiaji wa raslimali za ndani. Ofisi ya Rais Mipango inajukumu la kuchukua hatua za kubuni, kutekeleza na kusimamia sera zinazovutia uwekezaji wa mitaji kutoka nje ili kuhakikisha kunakuwa na matokeo endelevu yatakayo kuza uchumi na kupunguza umaskini.Sera hizi zinaweza kufanikiwa iwapo zitajikita katika kujenga na kuendeleza miundombinu ya umeme, maji, mawasiliano, barabara na reli. Eneo hili ni muhimu sana katika kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje.

ix) Eneo lingine muhimu ni utekelezaji wa sera zenye kujenga uwezo wa kutumia elimu ujuzi ufundi na teknolojia inayoandamana na uwekezaji kutoka nje kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani. Sera hizi zitafanikiwa kwa kujenga uwezo na ujuzi wa teknolojia ya kisasa kwa watanzania kupitia vyuo na tasisi mbalimbali za utafiti.

x) Kubuni na kutekeleza sera za kuvutia uwekezaji kutoka kwa Watanzania wanaofanya kazi nje.

xi) Kuna haja ya Ofisi ya Rais Mipango kuratibu uanzishwaji wa sera zenye kuwezesha watanzania kutafuta kazi katika soko la kazi la kimataifa. Mikakati ya kuhakikisha kuwa wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa zinashirikiana katika mambo yote yanyohusu uhamiaji na maendeleo ya watanzania waishio nje ya nchi. Mchango wa watanzania hawa ni muhimu katika ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini hasa kwa familia zao zilizopo hapa nchini na taifa kwa ujumla.

xii) Kuendeleza uwiano kati ya sera za uchumi huria na zile za kujitegemea

Sera za uchumi huria zinavutia biashara huria na uhuru wa usafiri wa mihimili ya uzalishaji kama vile mitaji na wafanyakazi.Sera hizi zinavutia uwekezaji mitaji na kuendeleza biashara ya kimataifa. Kwa upande wake sera za uchumi zisizohuria zinahimiza kujitegemea ,kuzuia biashara huria na uhuru wa kusafiri kwa mihimili ya uzalishaji. Ili kupata maendeleo ni vyema kukawepo na uwiano mzuri kati ya sera hizi mbili kwani sera za uchumi huria zinahitaji pia kusimamiwa kwa karibu ili nchi iweze kujenga uwezo wa kujitegemea.

## 10.5 Maoni na Mapendekezo ya Tume ya Mipango

Mapendekezo ya Tume ya Mipango ni kama ifuatavyo;

- Kuratibu mikakati na hatua za kuanzisha uchimbaji mkubwa wa madini kwa njia ya ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta za umma;
- Kufanya tafiti mtambuka zenye lengo la kubaini migongano ya sera inayozuia upatikanaji wa matokeo mazuri ya marekebisho ya kiuchumi, kijamii na kisiasa;
- Kufanya tafiti za kisera zenye kulenga katika kuongeza ufanisi wa raslimali za nje katika kuharakisha ukuaji wa uchumi;
- Kufanya tafiti itakayoweza kubaini namna ya kuweza kuwapatia watanzania wengi zaidi kazi katika soko la ajira la kimataifa na jinsi watanzania walio nje wanavyoweza kuongeza michango yao katika ukuzaji wa uchumi;
- Kufanya utafiti utakaosaidia kuleta uwiano mzuri kati ya matumizi ya raslimali kutoka nje na zile za ndani; na
- Kuelekeza misaada na mikopo kutoka nje katika sekta za uzalishaji